INTERNATIONAL TEACHERS TRAINING COLLEGE

1013/1 MK

KISWAHILI

Mock 1

February 2020

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

## PRIMARY TEACHER EDUCATION

## KISWAHILI LUGHA
(Karatasi ya 1)

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

(SIRI)

Kijitabu hiki kina kurasa 7 zilizopigwa chapa

## SEHEMU YA KWANZA

1. (a) Hii ni insha ya hotuba.

   (i) Insha iandikwe katika wakati uliopo katika nafsi ya kwanza.
   (ii) Hatibu awatambue wote waliohudhuria kwa vyeo vyao/atambue itifaki.
   (iii) Baadhi ya maadhui ni:

   - Utangulizi - Maamkizi/salamu kwa kuzingatia vyeo.
     - Kujitambulisha kwa jina, shule alimosomea, mwaka, kiwango cha elimu, kazi anayoifanya pamoja na wadhifa wake. Pia ataje kiini cha hotuba.

   - Mwili - Mambo muhimu ya kuzingatiwa na watahiniwa ni kama:

     (i) Kukamilishwa kwa mtaala.
     (ii) Matayarisho kabambe kupitia majadiliano katika vikundi, kujadili mada baada ya nyingine; kudurusu kwa kutumia maswali na majibu.
     (iii) Kutafuta usaidizi wa wanafunzi wenza na walimu.
     (iv) Kudumisha nidhamu shuleni ili kuepuka adhabu wakati wa mitihani ya shule na ya kitaifa.
     (v) Kutumia muda kwa njia mwafaka ili kujiepusha na hali ya wasiwasi wakati wa mtihani.
     (vi) Kujiamini kuwa unaweza.

   - Hitimisho - Kutoa ahadi za tuzo kwa watakaohitimu kwa alama za juu.
     - Kuwapa motisha kwa kuwahakikishia ushindi iwapo watazingatia maelezo yote uliyowapa.

   (b) Hii ni insha ya hoja.
   Baadhi ya hoja ni:

   (i) Wafanyikazi wakuu wa serikali kufanya kazi katika maeneo tofauti na walikozaliwa/mbali na makabila yao.
   (ii) Kuhimiza ndoa za mseto.
   (iii) Kuhimiza ajira ya watu kutoka kaunti tofauti, hasa kwa wale wanaohitimu masomo ya vyuo vikuu kwa mfano walimu na madaktari.
   (iv) Shule na vyuo kuhimizwa kusajili asilimia hamsini ya wanafunzi kutoka kaunti tofauti tofauti.
   (v) Serikali kuanzisha miradi inayohusisha makabila mbalimbali.
   (vii) Wakuu wa kaunti mbalimbali kuhimiza na kuandaa michezo na kaunti zingine.
   (viii) Maonyesho ya kilimo katika kaunti fulani yashirikishe kaunti zingine.
   (ix) Mtalaa uwe na somo au mada zinazoshughulikia haki na maridhiano nchini.
   (x) Ugavi wa nyadhifa katika serikali uzingatie watu kutoka maeneo yote nchini.
   (xi) Vyombo vya habari vitumiwe kuwahamasisha wananchi kuhusu faida na umuhimu wa utangamano na maridhiano.
   (xii) Wasanii mbalimbali wahimizwe na inapobidi wafadhiliwe katika kueneza ujumbe kuhusu utangamano na maridhiano.

(c) Hii ni insha ya methali.

Kisa kidhihirishe maana kuwa, iwapo mtu ananuia kutekeleza jambo fulani, anafaa kutumia mbinu yoyote itakayopatikana ili ajikimu bila kubagua.

(d) Hii ni insha ya mdokezo.

Insha imalizike kwa maneno yaliyotolewa.
Insha hii ina sehemu tatu:
(i) Kisa kionyeshe hali ya kutamausha hapo awali.
(ii) Bidii ya mhusika ibainike katika kubadilisha hali yake.
(iii) Mafanikio kutokana na bidii yake.

**Tanbihi**
(i) Mwanafunzi asiposhughulikia sehemu zote tatu, atakuwa amepungukiwa kimaudhui.
(ii) Iwapo hali ya kutamausha haitaonekana mwanzoni kabla ya kutia bidii, akadiriwe katika kiwango cha nusu.

## SEHEMU YA PILI

## MAJIBU - UFAHAMU

2. (a) (i) Nyenzo kuu ya mawasiliano.
(ii) Kipengele kikuu cha utamaduni.

(2 x 1 = 2)

(b) (i) Ukosefu wa sera madhubuti.
(ii) Upinzani kutoka kwa maadui wa lugha ya Kiswahili.
(iii) Matumizi ya lugha mbalimbali za kienyeji au kimaeneo.
(iv) Mawazo duni ya baadhi ya watu kuhusu Kiswahili; kukiona duni.
(v) Ushindani usiofaa kutokana na lugha nyingine za kimataifa.
(vi) Kukosa ufadhili katika uchapishaji wa kazi za kiswahili.
(vii) Mfumo uliopo wa masomo ni wenye kupendelea Kiingereza.
(viii) Ukosefu wa asasi za kudhibiti maendeleo na uenezaji wa lugha ya Kiswahili.

( 7 x 1 = 7)

(c) (i) Pawepo juhudi mpya za kuhamasisha raia kuhusu umuhimu wa Kiswahili.
(ii) Kuwe na asasi za kudhibiti maendeleo ya Kiswahili.
(iii) Serikali izue sera mwafaka za kukuza na kukieneza Kiswahili.
(iv) Kuwe na juhudi za kuwafanya raia kuionea fahari lugha ya Kiswahili.
(v) Kuhimiza matumizi bora ya Kiswahili katika vyombo vya habari kama vile redio na televisheni.
(vi) Raia kutumia Kiswahili ipasavyo katika shughuli mbalimbali.
(vii) Kiswahili kufunzwa shuleni na vyuoni.
(viii) Kiswahili kutumika katika mitandao ya kijamii.
(ix) Viongozi kuwa vielelezo katika matumizi ya Kiswahili.

(8 x 1 = 8)

(d) (i) Iligeuzwa/ilibadilishwa.
(ii) Kiswahili kilienea lakini kilikumbwa na changamoto.
(iii) Cheo/staha/heshima.

(3 x 1 = 3)

**SEHEMU YA TATU (alama 50)**

**MAJIBU**

3. (a) /e/ hutamkiwa sehemu ya kati ya ulimi /u/ ulimi huwa juu.
/e/ hutamkiwa sehemu ya mbele ya ulimi /u/ ulimi huwa nyuma.
/e/ midomo huwa imetandazwa ilhali /u/ midomo huwa mviringo
(2 x 1 = 2)

(b) Nyumba iliyojengwa imebomoka. (1 x 2 = 2)

(c) Simba alichomowa mkuki na msasi. (1 x 2 = 2)

(d) Maandishi haya hayasomeki. (1 x 2 = 2)

(e) Aliyakubali mawaidha ya wakuu wake. (1 x 1 = 1)

(f) Kijichaki chake kiliwekwa kwenye kijiguo/
Kichaki chake kiliwekwa kwenye kiguo.
(1 x 2 = 2)

(g) ni - kiulizi (1 x 1= 1)

(h) (i) kha! ni kihisishi kinachoibua bezo/dharau.
(1 x 1 = 1)
(ii) Huraa! ni kihisishi kinachobainisha ushindi/furaha/shangwe.
(1 x 1 = 1)

(i) Kubainisha **au/ama** kwa mfano: Tunahitaji jembe/uma humu shambani.
Kubainisha **maana sawa** kwa mfano Mama/nina amewasili.
Katika tarehe kwa mfano: Watafika tarehe 22/1/18
(yoyote 1 x 2 = 2)

(j) (i) Ku (1 x 1 = 1)
(ii) U-zi (1 x 1 = 1)

(k) (i) Atasafiri ughaibuni ilimradi apate matibabu. (1 x 1 = 1)
(ii) Hakusema wala kutenda lolote. (1 x 1 = 1)

(l) (i) Anayeheshimiwa ni huyu.
(ii) Huyu anaheshimiwa.
(yoyote 1 x 2 = 2)

(m) Walisema kuwa walikuwa wamebeba yote kwa hivyo ilikuwa sharti/ilibidi wapewe

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (n) | anakusudia - kitenzi kisaidizi | | (1 x 1 = 1) |
| | | kuimarisha - kitenzi kikuu | | (1 x 1 = 1) |
| | (o) | Yule mvivu amefukuzwa. | | (1 x 2 = 2) |
| | (p) | Marashi haya yananukia. | | (1 x 2 = 2) |
| 4. | (a) | (i) | halati | (1 x 1 = 1) |
| | | (ii) | jongo | (1 x 1 = 1) |
| | (b) | (i) | Vyombo vya kufanyia kazi fulani/ala. | |
| | | (ii) | Silaha na vyombo vya kutumia vitani. | |
| | | (iii) | Mzinga au sega la nyuki. | (2 x 1 = 2) |
| | (c) | niriki | | (1 x 1 = 1) |
| | (d) | Pesa anazopewa kijana mwanamume atokapo jandoni. | | (1 x 1 = 1) |
| | (e) | (i) | Purutangi | (1 x 1 = 1) |
| | | (ii) | Fuawe | (1 x 1 = 1) |
| | (f) | (i) | Takriri/urudiaji | (1 x 1 = 1) |
| | | (ii) | - Chuku<br>- Istiari | (1 x 1 = 1) |
| | (g) | Mlowezi/setla | | (1 x 1 = 1) |
| | (h) | Kuwa na tabia mbaya | | (1 x 2 = 2) |
| | (i) | Chapa ya umbo kama moyo aghalabu inayowekwa kwenye karata. | | (1 x 2 = 2) |
| | (j) | Ndege mdogo aliye na manyoya meusi kichwani na ya kijivujivu kifuani. | | (1 x 2 = 2) |
| | (k) | Nisamehe/kunradhi/samahani/naomba msamaha | | (1 x 1 = 1) |
| | (l) | mkono | | (1 x 1 = 1) |
| | | mguu | | (1 x 1 = 1) |

## SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA

5. (a) (i) Ni lugha iliyochaguliwa na serikali ili itumiwe katika mawasiliano rasmi /ya kiofisi. (1 x 2 = 2)

(ii) Ni matamshi ya mzungumzaji yanayotokana na lugha yake ya mwanzo au lugha zinazomzunguka. (1 x 2 = 2)

(b) (i) Hutumiwa kukuza lugha kwa kupanua msamiati kutokana ukwasi wake wa msamiati.

(ii) Husaidia kusanifisha lugha.

(iii) Huonyesha ukwasi wa lugha kupitia mitindo mbalimbali ya wazungumzaji na wandishi.

(iv) Huwakilisha historia ya lugha fulani.

(v) Hutumiwa kwenye fasihi kuonyesha uhuru wa mshairi.

(vi) Huipamba lugha hasa inapozungumzwa na wenyeji wake.

(vii) Ni kitambulisho cha jamii.

( 6 x 1 = 6)